**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA UCHUMI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,**

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kukutana leo hii kwa ajili ya kuendelea utekelezaji wa majukumu yetu ya kuwatumikia wananchi wetu. Nichukuwe fursa hii muhimu kukupongeza wewe binafsi mheshimiwa Spika kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu kwa ajili ya kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Uchumi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya (AR) Kazi, Uchumi, na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa masikitiko makubwa, naomba kutoa pole kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, pamoja na Wazanzibari wote kwa kuondokewa na aliyekua Makamo wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Hayati Maalim Seif Sharif Hamad. Hekima, Busara, Miongozo na Maoni yake yatabaki nasi katika

kuhakikisha upendo, mshikamano na umoja unaimarika ili kuleta tija na maendeleo kwa Wazanzibari. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amlaze mzee wetu mahali pema peponi. Ameen!!

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa huzuni kubwa, naomba pia kutoa pole kwa Watanzania wote kwa Kifo cha aliekua Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kilichotokea Tarehe 17 Machi, 2021. Milele tutamkumbuka kama kiongozi aliechukia na kupigana dhibi wa wala rushwa, na mwenye upendo wa kweli na Taifa lake. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ailaze roho wa mpendwa wetu, mahali pema peponi, Ameen!!

**Mheshimiwa Spika,**

Napenda kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru na kumpongeza kwa dhati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa umahiri wake wa kuiongoza nchi yetu kwa uadilifu wa hali ya juu unaopelekea wananchi kuzidi kujenga imani kwa Serikali. Tunawaomba waendelee kumuamini pamoja na kumpatia mashirikiano ya hali na mali hususan katika kuimarisha mazingira ya uwekezaji na kujenga miundombinu ya Uchumi wa Buluu kwa maendeleo ya nchi yetu.

Aidha, tunazidi kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kutekeleza ahadi zake alizozitoa katika Kampeni za Uchaguzi za mwaka 2020 alipokuwa akigombea nafasi ya Urais katika nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Nitumie fursa hii kutoa shukurani za pekee kwa Viongozi na Watendaji wote wa (AR) Kazi, Uchumi, na Uwekezaji pamoja na Taasisi zake kupitia Waziri wake Mheshimiwa Mudrik Ramadhan Soraga kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yao uliopelekea kutekeleza kwa asilimia kubwa malengo ya Wizara katika kipindi hiki kifupi tangu kuanza kwa Awamu ya nane ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Kamati inatoa shukurani za dhati kwa mashirikiano yao waliyotupatia na kutuwezesha kutekeleza majukumu ya Kamati kwa wepesi na ufanisi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa heshima ya kipekee na kwa kuthamini na kutambuwa michango na ushauri uliotolewa na Kamati yangu katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji. Naomba sasa niwatambue kwa kuwataja kwa majina Wajumbe wa Kamati ya Uchumi kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Shaaban Ali Othman - Mwenyekiti
2. Mhe. Sabiha Filifil Thani - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu - Mjumbe

4. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman - Mjumbe
5. Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf - Mjumbe
6. Mhe. Juma Makungu Juma - Mjumbe
7. Mhe. Hamza Hassan Juma - Mjumbe
8. Mhe. Hassan Hamad Omar - Mjumbe

Aidha, Kamati yetu inafanyakazi kwa karibu sana na makatibu wawili (2) ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakitusaidia kutekeleza majukumu yetu, kwa heshima naomba niwatambue kama ifuatavyo:

1. Ndugu Adam Maulid Simai - Katibu
2. Ndugu Asma Ali Kassim - Katibu

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu ilipitia makadirio ya Mapato na Matumizi ya fungu A07 la Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji mnamo tarehe 25/04/2021 katika ukumbi wa Kamati za Baraza la Wawakilishi. Kazi hiyo ilifanyika kwa ufanisi licha ya kuwepo kwa changamoto ya kuchanganyika lugha mbili za Kiswahili na Kiingereza katika vitabu vya fungu hilo. Hivyo, Kamati yangu inashauri (AR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji :

i. Kufanya maandalizi ya vitabu vya bajeti mapema
ii. Kufanya rejea ya vitabu hivyo kabla ya kuviwasilisha mbele ya Kamati

iii. Kufanya marekebisho ya kasoro za kilugha na kimaandishi zilizomo.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kulipitia fungu hilo, Kamati imebaini kuwa baadhi ya vifungu vya Wizara hii vinajirudia vikiwa na malengo yanayofanana na kupelekea msongamano wa vifungu. Hayo yanadhihirika katika (maelezo ya bajeti ya (AR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji ukurasa wa A07 –2). Kwa mnasaba huo, Kamati inapendekeza mpangilio mzuri uandaliwe ili kuingiza vifungu vinavyohitajika tu ambavyo ndio vinavyopaswa kuonekana kwenye bajeti ya Wizara hii ili viweze kuonekana kwa urahisi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa ruhusa yako na naomba niwasilishe mbele ya Baraza Lako Tukufu maoni ya Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilshi kuhusiana na Programu Kuu na Programu ndogo za (AR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 (AR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji inatarajiwa kukusanya jumla ya Tsh. 2,835,626,000 kupitia vyanzo mbalimbali vya mapato. Aidha, Wizara inakadiriwa kutumia jumla ya shilingi Tsh. 34,829,600,000 kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake. Kati ya fedha hizo shilingi Tsh.

13,864,600,000 ni za kazi za Kawaida na shilingi Tsh. 20,965,000,000 ni kwa ajili ya kazi za Maendeleo.

## PROGRAMU KUU YA KUSIMAMIA HUDUMA NA KURATIBU SHUGHULI ZA MHESHIMIWA RAIS NA KUIMARISHA MAWASILIANO IKULU

**Mheshimiwa Spika,**

Programu ya kusimamia huduma na kuratibu shughuli za Mheshimiwa Rais na kuimarisha mawasiliano Ikulu inakadiriwa kutumia jumla ya shilingi Tsh. 5,005,887,000 bilioni kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na inajumuisha programu ndogo mbili zifuatazo:

Programu ndogo ya kusimamia huduma na kuratibu shughuli za Mheshimiwa Rais inayokadiriwa kutumia jumla ya shilingi Tsh. 3,953,975,000 Bilioni pamoja na Programu ndogo ya Kuimarisha mawasiliano baina Serikali na Wananchi inayokadiriwa kutumia jumla ya shilingi Tsh. 1,051,912,000 Bilioni.

## PROGRAMU YA USIMAMIZI WA SHERIA ZA KAZI, UKAGUZI KAZI NA KAZI ZA STAHA KWA WOTE

**Mheshimiwa Spika,**

Programu ya usimamizi wa sheria za kazi, ukaguzi kazi na kazi za staha kwa wote imeundwa na programu ndogo tatu ambazo ni Uratibu wa upatikanaji wa ajira za

staha, usimamizi wa usalama na afya kazini na usimamizi wa viwango vya kazi vya kimataifa na majadiliano ya pamoja. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Programu hiyo inakadiriwa kutumia jumla ya Tsh. 2,236,900,000 bilioni. Kupitia fungu hili, Kamati yangu imeridhishwa na kiwango cha fedha zilizotengwa. Hivyo, kwa kuzingatia changamoto za ajira na uwepo wa migogoro mingi ya wafanyakazi katika kudai maslahi yao.

Kamati yangu inaishauri (AR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji kuzisimamia vyema sheria za kazi nchini ili kujenga mahusiano mema baina ya waajiri na waajiriwa sambamba na kuhakikisha kuwa inawalinda Wafanyakazi wa Kizanzibari pamoja na kupigania maslahi na stahiki zao.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamisheni ya Kazi hutoa vibali vya kazi kwa wataalamu wa kigeni ambao huhitajika katika sekta mbali mbali za kimaendeleo nchini. Kupitia huduma hiyo na huduma ya Ukaguzi katika sehemu za kazi ambao hutolewa kwa malipo. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 chanzo hicho kimekadiriwa kukusanya jumla ya shilingi Tsh. 1,005,626,000. Kiwango hicho ni upungufu ya shilingi Tsh. 786,221,000 milioni kutoka shilingi Tsh. 1,791,847,000 bilioni ambazo Wizara ilipangiwa kukusanya kupitia chanzo hicho kwa mwaka uliopita. Huu ni mwanzo mzuri na Kamati inaishauri (AR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji kutilia mkazo suala la ukomavu wa elimu kwa vijana wetu ili wawe wabobezi kwenye fani mbalimbali

hatimae wataalamu wa kigeni wapungue nchini mwetu ili kutoa fursa za ajira kwa vijana wetu Wazawa.

**Mheshimiwa Spika,**

Serikali kupitia Ilani ya uchaguzi ya 2020 – 2025 imeahidi ajira laki tatu kwa Wazanzibari. Kamati yangu imepata hofu na mashaka makubwa sana juu ya kutimia kwa ahadi hiyo ukizingatia kwamba (AR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji ambayo ndio yenye dhamana ya suala la ajira, imekadiria kutengeneza ajira 1,700 tu kupitia sekta binafsi kwa mwaka 2021 – 2022. Kamati inashauri (AR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji kujipanga upya, kuwa wabunifu na kufikiria kwa kina zaidi katika kipindi hiki ili kuongeza fursa za ajira nchini kwa nia ya kuisaidia Serikali kufikia azma hiyo.

**Mheshimiwa Spika,**

Malipo ya Ukaguzi kwenye sehemu za kazi ni chanzo chengine cha uhakika cha makusanyo ya Wizara kupitia Kamisheni ya Kazi ambapo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kimekadiriwa kukusanya jumla ya shilingi Tsh. 850,000,000. Kiwango hicho ni kidogo sana hasa ukizingatia kwamba (AR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji ina kitengo hafifu cha ukaguzi na nyenzo chache mno na kupelekea maeneo mengi kukosa kufikiwa kwa wakati. Hivyo, Kamati inashauri Wizara kutekeleza mambo yafuatayo:

i. Kuongeza wigo wa ukaguzi wa maeneo
ii. Kubuni mbinu bora zaidi za ukaguzi ili kuongeza mapato na kutunisha mfuko mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,**

Programu ndogo ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini inakadiriwa kutumia jumla ya shilingi Tsh. 120,000,000 milioni kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kwa ajili ya kuimarisha mfumo wa ukaguzi wa usalama na afya kazini. Kamati imeshangazwa na makadirio ya Wizara ya kutokea kwa ajali 8 za kikazi kwa mwaka 2021/2022. Kiwango hiki ni kikubwa kulingana na udogo wa nchi yetu na hivyo, Kamati inaishauri (AR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji kutoa taaluma kwa viongozi na watendaji kwenye taasisi za Serikali na sekta binafsi ili kupunguza ajali zinazoweza kutokea na kunusuru uharibifu wa watendaji na mali.

## PROGRAMU YA KUIMARISHA UWEKEZAJI NA SHUGHULI ZA SERIKALI KIKANDA NA KIMATAIFA

**Mheshimiwa Spika,**

Programu ya Kuimarisha uwekezaji na shughuli za serikali kikanda na kimataifa ina jumla ya programu ndogo tatu na inakadiriwa kutumia jumla ya shilingi Tsh. 10,599,601,000 bilioni kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Kupitia programu hii, Kamati inasisitiza umuhimu wa mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP) ili kuifungua Zanzibar kiuchumi na kujiletea maendeleo ya haraka.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Mradi wa Uimarishaji wa Maeneo Huru ya Micheweni unakadiriwa kutumia jumla ya shilingi Tsh. 1,000,000,000 bilioni. Kiwango hicho ni kidogo ukilinganisha na mahitaji halisi ya fedha za uendelezwaji wa maeneo hayo. Kamati inaiomba Serikali kuipatia (AR) Fedha na Mipango kutoa fedha hizo kwa wakati sambamba na (AR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji kuzitumia ipasavyo fedha hizo ili kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya barabara ambayo itawapa fursa wawekezaji kulifikia eneo hilo kwa ajili ya ukaguzi. Aidha, Kamati inashauri ujenzi wa miundo mbinu ya umeme, barabara na maji kufanyika kwa haraka ili kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, kwa maslahi ya Taifa letu na Wananchi wake.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, jumla ya shilingi Tsh. 20,965,000,000 zinakadiriwa kutumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya fungu A07 (AR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji. Kwa kweli kiasi hicho cha fedha ni kidogo na Kamati yangu inashauri kifungu hiki kuongezwa ili kukidhi shughuli za maendeleo ya Wizara.

**PROGRAMU YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI**

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imearifiwa kuwa mradi wa kuimarisha kituo cha Wanawake cha kutengeneza vifaa vya umeme wa jua (barefoot) umetengewa jumla ya shilingi Tsh. 965,000,000 kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Kiwango hiki cha fedha ni kikubwa kutokana na ukweli kwamba mradi hauendelei kuleta tija iliyokusudiwa kwa wanawake wanyonge wa visiwa vyetu kama ilivyokua hapo awali. Kwa upande wa Pemba, mradi umesimama kabisa na kuwaacha walengwa kwenye hali ya unyonge na kushindwa kujikimu kwa mahitaji ya msingi na familia zao. Kutokana na hali hiyo, Kamati inashauri tafiti za kina kufanyika kabla ya kuibuliwa miradi ili kujiridhisha iwapo miradi hiyo itakuwa na tija ya muda mrefu kwa jamii.

Pia, Kamati yangu inashauri (AR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji kufanya tathmini ya kutosha juu ya ulazima wa kutumika fedha hizo kwa tija zaidi ili kunusuru upotevu wa fedha za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa vile Kamati yangu imejadili kwa kina na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naomba sasa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili muijadili, mutoe ushauri pamoja na mapendekezo yenu na hatimae muiunge mkono bajeti hii. Kwa kumalizia, nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa niaba ya Kamati ya Uchumi na Wananchi wa Jimbo la Mpendae, naomba kuwasilisha.

Ahsante sana,

……………………..,

Shaaban Ali Othman,

Mwenyekiti

Kamati ya Kudumu ya Uchumi,

Baraza la Wawakilishi,

**Zanzibar.**